**TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Kumb.Na.13/KIST/CORR/VOL.XIV/173** **Tarehe: 12 Oktoba 2022**

# TANGAZO LA KAZI

## UTANGULIZI

Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia inatangaza nafasi mbili (02) za kazi kwa nafasi za Uongozi za Manaibu Wakuu wa Taasisi kama ifuatavyo;

## 1.1 NAIBU MKUU WA TAASISI UTAWALA, MIPANGO NA FEDHA

### SIFA ZA MUOMBAJI

1. Awe ni Mzanzibari mwenye kitambulisho cha ukaazi;
2. Awe na Shahada ya Tatu (PhD) katika fani ya Utawala, Uchumi, Sheria na fani yoyote inayolingana na hizo kutoka katika Taasisi inayoyotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
3. Awe na uzoefu wa kiutawala kwa angalau miaka mitatu (03) katika Taasisi ya kitaaluma;
4. Awe na ujuzi wa sheria na sera za kitaifa haswa katika Elimu na Utumishi wa Umma; na
5. Awe na maadili, muadilifu na mweledi kwa kuzingatia katiba ya nchi kuhusu uongozi.

### KAZI/MAJUKUMU

1. Atakua Msaidizi Mkuu na Mshauri Mkuu wa Mkuu wa Taasisi katika mambo yote yanayohusiana na utawala, mipango na fedha za Taasisi;
2. Atatekeleza majukumu mengine kama alivyokabidhiwa na Mkuu wa Taasisi kwa mujibu wamasharti ya Sheria ya Taasisi;
3. Kuratibu kazi za Utawala, Mipango na Fedha na Maendeleo katika Taasisi.
4. Kuhakikisha utayarishaji na utekelezaji kwa wakati wa makadirio ya bajeti ya Taasisi na bajeti ya uendeshaji.
5. Kuhakikisha udhibiti mzuri wa kifedha.
6. Atawajibika kwa Mkuu wa Taasisi kwa ajili ya usimamizi wa masuala ya wafanyakazi, mwenendo na nidhamu za wafanyakazi.
7. Atasimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi pamoja na miongozo inayotolewa naTaasisi;
8. Kuushauri Uongozi wa Taasisi ipasavyo na kwa haraka kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazotumika.
9. Atasimamia Idara zilizopo chini yake; na
10. Atasimamia mambo yote yanayohusiana na utawala, mipango na fedha kama itakavyoagizwa na Mkuu wa Taasisiau Baraza la Taasisi.

## 1.2 NAIBU MKUU WA TAASISI WA TAALUMA, UTAFITI, UBUNIFU NA USHAURI ELEKEZI

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe ni Mzanzibari na mwenye kitambulisho cha ukaazi;
2. Awe na Shahada ya Tatu (PhD) katika fani ya Sayansi na Teknolojia, au Uhandisi kutoka katikaTaasisi inayoyotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
3. Awe na maadili, muadilifu na mweledi kwa kuzingatia katiba ya nchi kuhusu uongozi;
4. Awe na uzoefu wa kiutawala kwa angalau miaka mitatu (03) katika Taasisi ya kitaaluma; na
5. Awe mbunifu na mwenye kufanya tafiti na kuweza kuchapisha makala kwenye majarida yanayotambulika pamoja na kutowa ushauri wa Kitaaluma.

**KAZI/MAJUKUMU**

1. Atakua mshauri Mkuu wa Taasisi juu ya mambo ya Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri Elekezi;
2. Kuratibu kazi za kitaaluma, utafiti, ubunifu na ushauri elekezi kwa Maendeleo ya Taasisi.
3. Kufanya tathmini na kushauri juu ya maendeleo ya kitaaluma katika Taasisi na kupendekeza programu mpya kwa kuzingatia mahitajika ya nchi.
4. Atawajibika kwenye masuala yote ya udhibiti ubora wa kitaaluma na udahili
5. Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi na miongozo inayotolewa na Taasisi;
6. Kusimamia Idara zilizopo chini yake;
7. Kupanga na kusimamia bajeti za idara zilipo chini yake.
8. Kuwasilisha matokeo ya mitihani kwenye Bodi ya Taaluma na kuyawasilisha katika Baraza laTaasisi;
9. Atawajibika kwa Mkuu wa Taasisi kwa ajili ya usimamizi wa masuala ya wanafunzi, mwenendo na nidhamu za wanafunzi.
10. Atakua kiungo miongoni mwa Idara; na
11. Kuwasilisha ripoti ya matokeo ya kila muhula katika mamlaka husika.

**NAMNA YAKUWASILISHA MAOMBI.**

Muombaji anatakiwa maombi yake ayafunganishe vizuri kwenye bahasha ikiwa ameambatanishana;

a) Barua ya maombi inayoonesha nafasi halisi anayoiomba, pamoja na Taarifa ya Maelezo binafsi (CV) yenye nakala sita (06).
b) Vivuli vya vyeti vya kumalizia masomo pamoja na matokeo yake.
c) Vyeti vya masomo kutoka nje ya nchi lazima vithibitishe na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania(TCU).
d) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.
e) Majina matatu ya wadhamini, taarifa zao za mawasiliano na ripoti za muombaji

zilizofungwa vizuri kwa usiri.

f) Picha tatu (Passport size) zilizopigwa karibuni.

g) Nambari ya Simu na barua pepe (e-mail).

h) Vivuli vitatu vya kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi.

**TANBIHI.**

1. Naibu Mkuu wa Taasisi wa Utawala, Mipango na Fedha na Naibu Mkuu wa Taasisi Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na wanaweza kuteuliwa kwa kipindi chengine cha miaka mitatu kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi.
2. Muombajia aanishe nafasi ya Uongozi anayoiomba, vyenginevyo maombi yake hayatozingatiwa.
3. Siku ya mwisho ya kupokea maombi ni siku ya **Ijumaa ya tarehe 21/10/2022 saa 9:30 Alaasir.**
4. Maombi yawasilishwe moja kwa moja Masjala ya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojiamuda wa saa za kazi pia unaweza kutuma kupitia barua pepe **info@kist.ac.tz** kwa wale waliokuwa nje ya nchi**.**
5. Mawasiliano yatafanywa kwa wale tu watakaotimiza vigezo (*shortlisted*).
6. Maombi yawasilishwe Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kwa anuani ifuatayo;

**MKUU WA TAASISI,**

**TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA,**

**S.L.P 476,**

**E-mail: info@kist.ac.tz**

**ZANZIBAR.**